kodi na makubaliano ya viwango katika makubaliano ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki 1994.

(4) Mapendekezo yatakayotolewa chini ya kifungu hiki yatazingatia misingi ya usimamizi wa mapato.

Kuzuia idhini

**31.**-(1) Pale ambapo Bunge limeridhika kuwa zipo sababu za kutosha zilizopelekea kushindwa kutekeleza kwa mapendekezo ya ukaguzi uliopita yaliyofanywa na Bunge, Bunge linaweza kuzuia matumizi ya kifungu maalum ndani ya Fungu, kutoka Mfuko Mkuu, kama takavyoona inafaa kwa madhumuni ya kugharamia matumizi ya Fungu hilo.

(2) Pale ambapo kwa hiari, Fungu hilo limekuwa kwa mfululizo likishindwa kutekeleza au kujibu hoja za ukaguzi na mapendekezo, Bunge linaweza, kwa mujibu wa taratibu za haraka utakavyoona inafaa, kuzuia fedha hizo kutoka katika Fungu hilo kwa mwaka kulingana na kiasi cha fedha kilichohojiwa kuhusu Fungu hilo.

(3) Pale ambapo Bunge limeridhika kuwa kwa hiari na mfululizo Fungu limeshindwa-

(a) kuzingatia misingi ya umakini na usimamizi mzuri wa fedha;

(b) kuzingatia misingi bora ya uhasibu na usimamizi wa fedha; au

(c) kufikia malengo na madhumuni ya bajeti linaweza, pamoja na taratibu nyingine itakavyoona ni za haraka, kuzuia kifungu kimoja au zaidi katika fundu kwa huduma mbalimbali katika Fungu hilo.

(4) Kutokana na kushindwa kwa mfululizo kwa Idara katika seksheni hii ambao unatokana na utendaji mbaya wa Afisa wa Umma, Bunge linaweza, kwa kura ya wachache, na kwa kuzingatia masharti kama itakavyoona inafaa, kuzuia mafano yoyote na mshahara wa Afisa huyo kwa muda itakavyoona inafaa.

(5) Pale ambapo Fungu linawasilisha mbele ya Bunge kuonesha kuwa limeyafanyia kazi mapendekezo ya ukaguzi wa hesabu, Bunge linaweza, iwapo sheria ya Fedha haijaidhinishwa, kuidhinisha malipo ya Fungu hilo kwa namna itakavyoona inafaa.

(6) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza, katika taarifa yake kwa Bunge, kupendekeza kuzuia matumizi ya kifungu chochote katika seksheni hii.

(7) Katika kifungu hii-

(a) 'kuzuia' ina maana kuzuia, kiasi Fulani au kiasi chote, kwa muda mfupi au moja kwa moja, kifungu kimoja au zaidi ambacho kipo katika makadirio ya mwaka; na

(b) fungu, linajumuisha Wizara au Taasisi ya Umma.

Serikali kukiuka malengo ya kibajeti

**32.**-(1) Serikali inaweza, kwa idhini ya Bunge, kukiuka malengo ya kibajeti kutoka katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa muda mfupi pale ambapo ukiukaji huu unatokana na majanga ya asili au tukio linguine jingine ambalo halikutarajiwa kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 35.

(2) Pale ambapo yapo mabadiliko ya Serikali, Serikali mpya inaweza, kwa idhini ya Bunge, kukiuka malengo ya kibajeti katika Mwongozo wa Mpango wa Bajeti bila ya kukiuka misingi ya bajeti.

(3) Waziri atawasilisha bungeni taarifa ya ukiukaji wa malengo ya bajeti, na atajumuisha katika taarifa hiyo-

(a) sababu na matokeo ya ukiukaji huo;

(b) mapendekezo ya kushughulikia uhamisho huo;

(c) muda unaokisiwa wa mabadiliko haya; na

(d) hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoanzishwa na Serikali na iwapo kuna mradi uliosimamishwa, na sababu za kufanya hivyo.

Vyanzo vya Mfuko wa Dharura

**33.**-(1) Mfuko wa Dharura ulioanzishwa utajumuisha fedha zilizotengwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Sheria ya Fedha katika kila mwaka wa fedha.

(2) Mfuko wa Dharura utarejeshewa kila mwaka kwa kiwango kilichoidhinishwa hapo awali katika bajeti ya mwaka uliopita.

(3) Mfuko wa Dharura utakuwa sehemu ya Bajeti ya mwaka na Bunge, pamoja na viwango vilivyotajwa katika kifungu kidogo cha (2), litaidhinisha fedha nyingine kwa kadri litakavyoona inafaa.

Sura 418

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi, atatoa taarifa katika Bunge kuhusu hesabu za Mfuko wa Dharura.

Waziri kusimamia Mfuko wa Dharura

**34.**-(1) Waziri atasimamia Mfuko wa Dharura.

(2) Kiwango cha Kudumu cha Mfuko wa Dharura hakitazidi kiwango kilichoelezwa na Waziri baada ya kuidhinishwa na Bunge.

(3) Waziri atatunza Mfuko wa Dharura katika akaunti tofauti, katika Benki Kuu ya Tanzania na-

(a) atafanya malipo kwenye akaunti ya mfuko wa dharura kutoka kwenye mfuko wa Serikali kupitia sheria ya kuidhinisha matumizi ya fedha; na

(b) atalipa kutoka mfuko wa dharura bila kuchelewa, matumizi yote kwa mujibu wa kifungu cha 35.

Matumizi kutoka Mfuko wa Dharura

**35.**-(1) Waziri anaweza kutoa fedha kutoka Mfuko wa Dharura pale ambapo, kwa msingi wa vigezo vilivyowekwa na mfumo na taratibu za mwongozo wa uendeshaji zilizotajwa na kuidhinishwa na Bunge pamoja na sheria kuhusiana na kudhibiti majanga akiridhika kuwa ipo dharura na jambo lisilotarajiwa na kusababisha umuhimu wa kufanya matumizi ambayo hayamo katika sheria yoyote maalum.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Waziri kwa kuongozwa na Sheria na Kanuni zilizopo, amethibitisha kuwa-

(a) malipo hayakukasimiwa katika bajeti kwa sababu hayakutarajiwa na hayawezi kusubiri mpaka mwaka ujao wa fedha bila kuathiri manufaa kwa umma; na

(b) tukio halikutegemewa.

(3) Pamoja na Kanuni na Sheria husika, kwa madhumuni ya Seksheni hii, tukio lisilotegemewa ni lile ambalo-

(a) linatishia kwa kiasi kikubwa uhai na ustawi wa binadamu;

(b) linatishia uharibifu mkubwa wa mazingira; na

(c) linahusisha kuokoa uharibifu, hasara, ugumu, mateso yanayosababishwa moja kwa moja na tukio hilo.

(4) Tukio litachukuliwa kwamba linatishia uhai wa binadamu au ustawi pale tu linapohusisha, kusababisha au linaweza kusababisha-

(a) kupotea kwa uhai, ugonjwa wa binadamu au maumivu;

(b) kukosa makazi au uharibifu wa mali;

(c) kuvurugwa kwa huduma, ikiwamo huduma ya afya.

(5) Fedha katika Mfuko wa Dharura zinatunzwa kwa matumizi ya majanga ya asili zinaweza kutumika

kumuokoa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameathiriwa na majanga ya asili yaliyotokea nje ya Jamhuri ya Muungano, pale ambapo masharti ya kifungu kidogo cha (1) yamezingatiwa.

(6) Mchango wa fedha kwenda katika Fungu, kuhusu majanga ya asili, utatangazwa na Waziri ndani ya siku thelathini baada ya kupokea taarifa.

(7) Kwa kuzingatia kifungu kidogo (2), Waziri, kwa mujibu wa kanuni na idhini ya Bunge, ataweka vigezo vya kutoa fedha kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1).

Bunge kuidhinishwa kwa fedha zilizotumika kutoka Mfuko wa Dharura

**36.**-(1) Waziri, ndani ya miezi miwili baada ya kufanya malipo kutoka Mfuko wa Dharura atawasilisha Bungeni taarifa ya kina kuhusu malipo yaliyofanyika akizingatia mahitaji ya taarifa yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha 37(2) na kupata idhini ya Bunge kuhusu malipo hayo.

(2) Pale ambapo Bunge halikutani katika kipindi kilichotajwa katika kifungu kidogo (1), au halitakutana katika mwisho wa kipindi hicho na Waziri hajaomba idhini ya Bunge kabla ya kipindi hicho kuisha. Waziri ataomba idhini hiyo ndani ya siku kimi na tano baada ya Bunge lijalo kuketi.

(3) Mara tu baada ya Bunge kuidhinisha malipo, Waziri atawasilisha Muswada wa Fedha kupelekwa Bungeni kupata idhini ya fedha zilizotolewa ziweze kurudishwa katika Mfuko wa Dharura kwa kiasi kilichotumika.

Taarifa za Fedha kuhusu Mfuko wa Dharura

**37.**-(1) Waziri, ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa za fedha za mwaka huo kuhusiana na Mfuko wa Dharura.

(2) Waziri atajumuisha taarifa zifuatazo katika taarifa za fedha zinazoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

(a) tarehe na kiasi cha kila malipo yaliyofanyika kutoka Mfuko wa Dharura;
(b) mtu ambaye kwake malipo yamefanyika;
(c) madhumuni ya kufanya malipo hayo;
(d) iwapo mtu ambaye malipo yamefanyika kwake ametumia fedha hizo kwa madhumuni hayo, taarifa kuhusu hilo;

(e) iwapo mtu ambaye malipo yamefanyika kwake, bado hajatumia fedha hizo kwa madhumuni hayo, taarifa kuhusu sababu za kutofanya hivyo; na

(f) taarifa ya kuonesha ni kwa namna gani malipo yamezingatia vigezo vya kufanya malipo hayo.

Mapato na Uwekezaji

**38.** Fedha hazitaingia katika Mfuko wa Dharura isipokuwa zile ambazo zimeidhinishwa kwa Sheria ya Bunge pamoja na riba au mapato mengine ambayo yanaweza yakaingizwa katika Mfuko wa Dharura na fedha hizo zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Uhamisho wa Fedha

**39.**-(1) Afisa Masuuli anaweza, baada ya kupata idhini ya Waziri, atahamisha fedha kutoka matumizi yaliyoidhinishwa.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo (1), Afisa Masuuli hatafanya uhamisho wa fedha pale ambapo-

(a) Fedha hizo zimeidhinishwa kwa matumizi ya ofisi nyingine ya Serikali au mtu;

(b) fedha zimeidhinishwa kwa matumizi ya uwekezaji to defray matumizi mengine ya maendeleo;

(c) uhamisho wa fedha ni kutoka katika mishahara kwenda katika matumizi yasiyo ya mishahara; au

(d) uhamisho wa fedha unaweza kusababisha kuvuruga misingi ya bajeti.

(3) Afisa Masuuli anaweza kufanya uhamisho wa fedha za miradi kati ya mafungu katika bajeti ya mwaka wa fedha, iwapo-

(a) vipo vifungu katika bajeti za miradi ya mafungu ambavyo vinaweza visitumike;

(b) maombi ya uhamisho wa fedha yamewasilisha hazina yakitoa maelezo ya ufafanuzi kuhusu uhamisho wa fedha na Hazina imeidhinisha maombi hayo; na

(c) Kiwango cha jumla cha uhamisho wa fedha kulikofanywa kwenda au kutoka katika miradi au mafungu kwa kiwango kisichozidi matumizi yaliyoidhinishwa katika mradi huo au mafungu katika mwaka huo wa fedha.

(4) Waziri anaweza, kwa kanuni, kuidhinisha uhamisho wa fedha ndani ya bajeti za mafungu yaliyoidhinishwa na uhamisho wa fedha ndani ya mafungu

au miradi.

(5) Mamlaka ya Waziri katika uhamisho wa fedha katika bajeti hayatekelezwa-

(a) kiwango cha fedha katika mafungu tofauti;

(b) kutoka matumizi ya maendeleo kwenda matumizi ya kawaida. Isipokuwa, uhamisho umeidhinishwa kwa bajeti ya nyongeza, na hauzidi kiwango kilichoidhinishwa katika Fungu.

(6) Afisa Masuuli anaweza kuhamisha fedha za ndani ya Fungu bila ya kupata idhini ya Waziri kwa kiwango cha asilimia kilichoidhinishwa katika kanuni na kutoa taarifa kwa Malipaji Mkuu wa Serikali katika kila robo ya mwaka kuhusu uhamisho huo.

(7) Uhamisho wowote wa fedha:-

(a) utafanyika kwa kushauriana na Wizara zote zilizoathirika pamoja na Taasisi za Serikali; na

(b) utawasilishwa Bungeni na kutolewa taarifa kila robo mwaka.

Mapato ya ziada

**40.**-(1) Mapato yote yaliyokusanywa zaidi ya kiwango kilichotajwa katika makadirio kitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(2) Taarifa ya matumizi ya ziada itatakasishwa na taarifa ya Afisa Masuuli husika ikielezea sababu za matumizi ya ziada na hatua za kuchukua kuzuia matumizi hayo ya ziada yasitokee.

Kuwasilisha Bajeti ya Nyongeza

**41.**-(1) Serikali itawasilisha Bungeni kwa idhini, bajeti ya nyongeza ya fedha zilizotumika ambazo zimezidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge au kwa madhumuni ya kugharamia mahitaji ambayo hayakupangwa.

(2) Bajeti ya Nyongeza itahitajika kwa-

(a) kuongeza au kupunguza katika idhini mabadiliko ya malengo, au kupata idhini mpya katika sheria ya fedha.

(b) kuongeza au kupunguza kiwango cha line item katika makadirio iwapo hayataweza kufikiwa katika mabadiliko ya fedha au mabadiliko ya matumizi yake.

(c) kuonesha namna ambayo Mfuko wa Dharura umetumika.

(3) Pale ambapo Bunge limeidhinisha matumizi, Sheria ya Fedha itapitishwa kwa kiwango kilichoidhinishwa.

(4) Bajeti ya Nyongeza itajumuisha taarifa ya matumizi ya ziada na mapato husika katika kipindi hicho katika kutekeleza misingi ya fedha na Bajeti.

## SEHEMU YA TANO
## UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA WA BAJETI

Mamlaka ya Matumizi

**42.** Mahali ambapo Serikali na taasisi na mashirika ya umma yanakuwa na matumizi yanayotokana na Mfuko Mkuu chini ya Sheria ya Bunge:-

(a) Afisa Mhasibu ana mamlaka ya kutumia fedha kadri ya sababu zilizobainishwa katika sheria; na

(b) Mgawo wa fedha kwenye mafungu utazingatia utekelezaji, bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha.

Idhini ya kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu

**43.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, kwa mamlaka aliyopewa, atatoa idhini ya kutumia fedha za Mfuko Mkuu kwa Waziri.

(a) Kiasi kinachotakiwa kulipwa katika miezi mitatu inayofuatia kwa ajili ya matumizi ya kisheria; na

(b) Kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa huduma za mwaka wa fedha chini ya mamlaka ya Sheria ya Matumizi.

Utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu

**44.** (1) Malipo hayatafanywa –

(a) kutoka kwenye Mfuko Mkuu isipokuwa namna itakavyotolewa na sheria iliyoandikwa; na

(b) zaidi ya kiasi ambacho kimetolewa chini ya matumizi kwa huduma yoyote.

(2) Kwa kuzingatia vipengele vya sheria inayohusiana na matumizi ya Serikali itatumika kuhusiana na utoaji wa fedha kutoka kwenye Mfuko Mkuu.

Kibali cha Mhasibu Mkuu

**45.**-(1) Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa kibali alichonacho atawaidhinisha maafisa masuuli kufanya matumizi hadi kufikia kiwango kwa madhumuni na kwa kuzingatia masharti yaliyomo kwenye kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali.

(2) Kibali hakitatolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali mpaka pale kiasi na makusudi ambayo yamesabisha kutolewa yamebainishwa katika kibali kilichotolewa na Mlipaji Mkuu.

(3) Kila kibali kitakachotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kitazingatia kiwango na masharti ambayo Waziri atayaainisha.

(4) Afisa Masuuli anaweza asifanye malipo yoyote au kukubali kulipa kutoka kwenye akaunti au kuingia miadi yoyote au matumizi, isipokuwa imeidhinishwa kwa kibali kufanya hivyo.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo (4) "miadi" maana yake mkataba, makubaliano au mpangilio kwa ajili ya kufanya malipo.

Dhana ya miadi

**46.** Taasiri au Mashirika ya Umma itafanya miadi chini ya masharti yafuatayo-

(a) Kiasi ambacho kitalipwa chini ya miadi ni sawa na au pungufu ya kiasi kilichopo kwa ajili ya matumizi;

(b) Uhalali wa malipo yatakayofanywa chini ya miadi itakuwa imehakikiwa; na

(c) Miadi ni kwa mujibu wa matoleo ya fedha ya bajeti ya robo mwaka.

Miadi ya miaka mingi

**47.**-(1) Miadi yoyote ya miaka kadhaa itahitaji kwanza kupata kibali cha Waziri.

(2) Kupata kwanza kibali cha Waziri kunahitajika kwa ajili ya kuhakikisha kuwa-

(a) miadi haisababishi ukomo wa matumizi ya miaka kadhaa chini ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti;

(b) kiasi ambacho kinatakiwa kulipwa chini ya miadi katika mwaka uliopo wa fedha kinatakiwa kiwe sawa au pungufu kuliko kiasi kilichopo kwa ajili ya matumizi;

(c) uhalali wa malipo yatakayofanyika chini ya miadi ini budi yawe yamehakikiwa; na

(d) sehemu ya miadi inayotakiwa kulipwa kwa mwaka husika wa bajeti ni sawa na robo ya bajeti iliyotolewa kama ipo.

Mfumo wa udhibiti wa miadi

**48.**-(1) Serikali na Taasisi na Mashirika ya Umma yatahitajika-

(a) kutunza mifumo ya udhibiti wa miadi ambapo miadi yote inayodhaniwa itaingizwa; na

(b) kuzuiwa malipo kufanyika kutoka kwenye bajeti bila ya miadi ya msingi kuwa imeingizwa kwenye mfumo wa udhibiti wa miadi na namba ya miadi kutolewa na mfumo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo (1), miadi yote ambayo haijatekelezwa itajumuishwa kwenye makadirio ya mwaka yakionesha-

(a) ikuna kiasi cha kutosha kwenye kipengele ili kikidhi miadi ya miaka kadhaa ambayo haijatekelezwa ambayo italipwa chini ya kipengele husika; na

(b) ukomo wa matumizi na maoteo ya kibajeti chini ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti yanaakisi kikamilifu miadi ya miaka kadhaa.

Mikataba ya Miradi ya Maendeleo

**49.**-(1) Taasisi na Mashirika ya Umma yatakikiwa kwanza kupata kibali cha Waziri kabla ya kuingia kwenye mikataba yenye mahitaji ya kifedha.

(2) Waziri anaweza kutoa idhini ya kifedha kwa masharti kwamba mkataba unatimiza vigezo vya miadi ya miaka kadhaa na mradi unawezekana kwa maoni ya Waziri.

Taarifa za ndani ya mwaka

**50.**-(1) Mhasibu Mkuu wa Serikali ndani ya muda uliobainishwa kwenye Kanuni atatakiwa, atawasilisha kwa Katibu Mkuu, taarifa ya Serikali na taasisi na mashirika ya umma kuhusiana na mapato na matumizi halisi kwa mwezi uliopita na kiasi ambacho kinatarajiwa kukusanywa au kutumika katika mwezi huo na Serikali.

(2) Taasisi na mashirika ya umma, mifuko maalum, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii itatoa taarifa kwa Mlipaji Mkuu kuhusu mapato na matumizi katika kila robo mwaka.

(3) Kamishna wa Bajeti kwa kushirikiana na Kamishna wa uchambuzi wa sera, ndani ya muda utakaoelezwa na kanuni watachapisha taarifa utekelezaji wa bajeti ya robo mwaka.

(4) Maafisa Wahasibu, ndani ya muda utakaoelezwa kwenye kanuni atawasilisha taarifa ya utekelezaji ya robo mwaka kwa Katibu Mkuu Hazina.

Taarifa za Utekezaji

**51.**-(1) Waziri, ndani ya miezi mitatu baada ya kuwasilisha bajeti kwenye Bunge na katika kila robo mwaka baada ya hapo atawasilisha kwenye Bunge, kwa mtiririko na kwa ujumla taarifa ya utekelezaji.

(2) Wakati Bunge halipo kwenye vikao vyake na katika zilizobainishwa kwenye kifungu kidogo (1) taarifa ya utekelezaji itawasilishwa katika Bunge katika siku ya pili, mara tu baada ya kuanza kwa Bunge.

(3) Taarifa ya Utekelezaji-

(a) itaonesha kipindi cha mapitio, na jinsi ambavyo malengo na shabaha katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti yamefikiwa; na

(b) kubainisha kiasi kifuatacho na kuvilinganisha na

shabaha zinazoendana katika kipindi cha mapitio-

(i) mapato halisi katika kipindi husika na ikilinganishwa wa matarajio;

(ii) matumizi halisi kwa fungu, yakitofautishwa baina ya matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa kipindi hicho; na

(iii) mikopo halisi kwa kipindi hicho, na kwa mwaka wa fedha hadi mwisho wa mwaka wa fedha.

(4) Ambapo malengo na shabaha hayajafikiwa, taarifa ya kisheria itataja-

(a) sababu za kwa nini malengo na shabaha hazikufikiwa;

(b) hatua za marekebisho zinachukuliwa kuhakikisha kuwa malengo na shabaha ambayo hayakufikiwa yatafikiwa katika robo ijayo; na

(c) Mapendekezo yoyote ya maamuzi ya kisera ya Serikali ambayo yanaweza kuathiri kwa kiwango kikubwa malengo na shabaha katika taarifa ya matarajio ya bajeti au utekelezaji wa kibajeti na kiuchumi kwa ujumla katika nchi.

(5) Mhasibu Mkuu wa Serikali, ataandaa taarifa ya kila mwezi ya Mfuko Mkuu ambayo itahusisha mapato halisina ridhaa za matumizi zilizotolewa na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu ili kutumika katika maandalizi ya taarifa mbalimbali.

Taarifa za Serikali za robo mwaka

**52.**-(1) Mhasibu Mkuu wa Serikali ataandaa taarifa ya mapato na matumizi halisi kwa ujumla wake ya Serikali na Taasisi na Mashirika ya Umma na kuwasilisha kwa Waziri ambaye atawasilisha kwenye Bunge mwezi mmoja baada ya mwisho wa kila robo mwaka.

(2) Afisa Masuuli ataandaa na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali taarifa za uhamisho wa fedha uliofanyika ndani ya Mafungu husika.

## SEHEMU VI
## USIMAMIZI WA MAPATO

Misingi ya usimamizi wa mapato

**53.**- Sehemu ya Mapato ya Bajeti itazingatia misingi ifuatayo-

(a) mapato yote ya Serikali kutoka vyanzo vya ndani na nje yataingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina;

(b) yeyote aliyepewa mamlaka ya kukusanya mapato

ya Serikali atawajibika katika ukusanyaji wa mapato wenye ufanisi, na utunzaji hesabu na utoaji taarifa kwa kuzingatia sheria husika na kuchukua tahadhari ili kuzuia ufujaji wa mapato ya Serikali;na

(c) mapato yote ya Serikali yataingizwa kwenye Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali.

Majukumu ya Ukusanyaji Mapato na Usimamizi

**54.**-(1) Waziri ataweka utaratibu wa kupokea maoni na mapendekezo kuhusu makadirio ya bajeti kwa mwaka ujao wa fedha kutoka kwa Bunge ambayo yatawasilishwa kwa Waziri si zaidi ya tarehe 15 Februari.

(2) Majukumu ya Katibu Mkuu kuhusiana na ukusanyaji na usimamizi wa mapato yatakuwa ni-

(a) kusimamia na kuweka misingi ya mipango na utafiti wa vyanzo vya mapato vya sasa na fursa ya mapato zaidi zilizopo;

(b) kuanzisha mfumo ambao utaweka muda maalum wa kupokea mapendekezo ya hatua za mapato;

(c) kuandaa hatua za mapato kwa bajeti ya Serikali;

(d) kutafuta rasilimali ikiwa pamoja na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kujumuisha fedha hizo kwenye michakato ya mipango, bajeti na utoaji taarifa na uwajibikaji kama inavyoelezwa na sheria hii.

(e) kuboresha na kusimamia uwazi, ufanisi na namna inayofaa ya usimamizi wa mapato;

## SEHEMU YA SABA
## USIMAMIZI WA VIFUNGU VIDOGO NA SERIKALI NA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

Usimamizi wa kibajeti na kifedha za Serikali za Mitaa

**55.**-(1) Waziri atasimamia masuala ya kibajeti na kifedha ya mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) bajeti inayopendekezwa na bajeti zilizoidhinishwa kwa pamoja zitawasilishwa kwa Waziri kwenye dhamana ya mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia muda maalum.

(3) Uanzishwaji na usimamizi wa asasi zinazofanya kazi nje ya mfumo wa bajeti na mifuko maalum ya Serikali za Mitaa kutahitaji idhini ya Waziri wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Usimamizi wa kibajeti na kifedha na wa asasi nyingine za Serikali

**56.**-(1) Waziri mwenye dhamana usimamizi wa kibajeti na kifedha na asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti na Mifuko Maalum inayojumuishwa ndani ya Serikali Kuu na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) bajeti inayopendekezwa na bajeti iliyoidhinishwa ya asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti na Mifuko inatakiwa kuwasilishwa kwa Waziri na Waziri mwenye dhamana kwa kuzingatia muda maalum ulioelezwa kwenye Kanuni;

(b) mikopo kwa ajili ya asasi zilizo nje ya mfumo wa bajeti na Mifuko maalum itahitaji kupata kwanza kibali cha Waziri, endapo asasi hiyo iliyo nje mfumo wa bajeti ina uwezo huo kisheria.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI YA JUMLA

Kanuni na Maelekezo

**57.**-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni zinazohitajika kuwezesha utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti kifungu kidogo (1), kanuni zitakazotungwa zibaainisha-

(a) yaliyomo na aina mbalimbali ya taarifa zinazohitajika na Sheria hii;

(b) muda wa kufuata kuwasilisha taarifa kabla ya kuwasilisha Bungeni;
(c) vigezo ambavyo Bunge litatumia kuamua endapo hoja za ukaguzi zimezingatiwa; na
(d) kanuni au vigezo vitakavyotumika kubainisha mgao wa fungu haukuzingatia sheria hii.

Kuongeza Kipindi cha muda uliowekwa

**58.** Bunge linaweza kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa au nyaraka zinazotakiwa kuwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Sheria hii au muda uliowekwa kikatiba kupitia azimio.

Uwajibishaji wa Mamlaka iliyoshindwa kutekeleza matakwa ya Sheria

**59.**-(1) Serikali na taasisi za umma zitakaposhindwa kutekeleza masharti ya Sheria hii, Waziri atalazimika kutoa maelezo na mazingira yaliyosababisha kushindwa kutekeleza masharti husika.

(2) Endapo inapothibitika kwamba afisa wa umma kwa kusudia au kwa uzembe amesababisha Serikali au taasisi ya umma kushindwa kutekeleza masharti ya Sheria hii, Afisa huyo atakuwa ametenda kosa la kinidhamu na atachukuliwa hatua za kinidhamu na atawajibishwa yeye mwenyewe.

(3) Waziri atachukua hatua za kurekebisha taasisi ya umma pale inaposhindwa kufuata taratibu za kifedha au matumizi za ziada au matumizi ambayo hayajaidhinishwa.

(4) Hatua za kurekebisha zinazoainishwa katika kifungu kidogo cha (3) zitajumuisha:
(a) kuwasilisha na kuidhinisha Mpango kazi;
(b) kupunguza kiasi cha bajeti iliyotumika zaidi ya iliyoidhinishwa katika mwaka unaofuata wa fedha;
(c) kuweka sharti la Waziri kuomba kibali kabla ya kufanya matumizi; na
(d) kusitisha mamlaka ya Afisa Masuuli katika usimamizi wa fedha.

Hatua za urekebishaji dhidi ya Serikali na Taasisi za Umma

**60.**-(1) Waziri atachukua hatua za kurekebisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi iliyopo nje ya bajeti ya Serikali na mfuko maalum ikiwemo Serikali, taasisi ya umma, pale Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi iliyopo nje ya bajeti ya Serikali na mfuko maalum itakaposhindwa kufuata taratibu za kifedha au matatizo ya kifedha.

(2) Hatua za kurekebisha zitajumuisha-

(a) Kuwasilisha Mpango wa Utekelezaji;
(b) Kuweka sharti la Waziri kuomba kibali kabla ya kufanya maamuzi;
(c) Kupunguza au kusimamisha uhamishaji wa fedha za bajeti; au
(d) Kuteua msimamizi wa fedha ambaye atakuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi.

Hatua dhidi ya Maafisa wa Umma

**61.** Afisa wa umma aliyepo Serikalini, taasisi ya umma,Taasisi iliyopo nje ya bajeti ya Serikali na mfuko maalum hatachukuliwa hatua mwenyewe za kiutawala au za makosa ya jinai kwa kufanya au kuacha kufanya kwa nia nzuri wakati wa utekelezaji au alipotakiwa kutekelezaji wajibu aliopewa au wakati wa utekelezaji wake wa majukumu aliyopewa kwa mujibu wa Sheria hii na nafasi yake ya kazi.

Masharti ya Sheria kuwa na mamlaka ya juu

**62.** Sheria hii itakuwa na masharti ya mamlaka ya juu dhidi ya sheria nyingine katika masuala yoyoyte yanayohusu-

(a) bajeti ya taifa, bajeti ya taasisi za umma, mamlaka za serikali za mitaa au wakala nje ya bajeti;
(b) usimamizi wa mchakato wa bajeti;
(c) utekelezaji, ufuatiliaji. Tathimini na utoaji wa taarifa wa bajeti;
(d) usimamizi wa mapato na matumizi ya bajeti; na
(e) kusimamia taasisi za umma na wakala nje ya bajeti.

Masharti ya Mpito

**63.**-(1) Sheria hii itakapoanza kutumika, fungu husika kwa ajili ya mafungu mbalimbali ambazo bado hazijawasilishwa kwa kuzingatia taarifa au utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi zitaanza kutumika siku baada ya makadirio kuwasilishwa Bungeni.

(2) Mafunguyataomba kiasi kinachotakiwa kwa ajili ya kukidhi matumizi muhimu ya shughuli za Serikali na taasisi za umma kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka huo.

(3) Bunge litaweka ukomo wa kiasi kitakachoidhinishwa kwa fungu husika kwa asilimia ishirini na tano au chini ya kiasi chote kilichopo katika makadirio ya mwaka endapo anayeomba vote hajatekeleza masharti ya kifungu cha 64.

(4) Katika kifungu hiki, "shughuli za Serikali" zitamaanisha huduma zozote zinazotolewa na kazi zinazofanywa na fungu ikiwa huduma hizo ni za kawaida au sio za kawaida.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Bajeti kwa lengo la kuweka mfumo wa kisheria utakaosimamia mchakato wa Bajeti ya Serikali kuanzia uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathimini na utoaji taarifa.

Muswada huu unakusudia kuweka mfumo bora wa kiutendaji kati ya Serikali, Bunge na vyombo vingine vinavyohusika katika mchakato wa bajeti, kuwepo kwa nidhamu ya bajeti kwa kuweka misingi ya kuzingatia mipango, mapato na matumizi, kuwepo kwa bajeti inayoaminika yenye kuzingatia utekelezaji kama ilivyoidhinishwa na Bunge pamoja na kuweka utaratibu maalum wa kufanya uhamisho wa fedha. Aidha, Muswada huu unatarajia kujumuisha Bajeti za Wakala na Taasisi za Serikali katika Vitabu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ili kuonyesha uwazi wa bajeti zao na jinsi zinavyochangia katika kukua kwa Uchumi wa Taifa.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nane.

Sehemu ya Kwanza inaainisha masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Sheria, kipindi cha kuanza kutumika kwa Sheria, matumizi ya Sheria ambapo Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya Sheria.

Sehemu ya Pili inabainisha masuala ya muundo wa mfumo wa Uchumi Jumla na bajeti. Aidha, sehemu hii inabainisha misingi ya sera za bajeti, malengo ya sera za bajeti, matarajio ya Uchumi Jumla na bajeti na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Sehemu ya Tatu inabainisha mamlaka zitakazohusika katika usimamizi wa mfumo wa bajeti ya Serikali kati ya Bunge na Serikali ambapo mamlaka na majukumu yao yamebainishwa yakiwemo ya Waziri wa Fedha, Waziri wa Tume ya Mipango, Katibu Mkuu Hazina, Kamishna wa Bajeti, Kamati ya Kitaifa ya Uandaaji Mwongozo wa Bajeti, Kamishna wa Uchambuzi wa Sera, Msajili wa Hazina na Maasifa Masuuli.

Sehemu ya Nne inabainisha masuala ya uandaaji wa Bajeti ya Serikali na uidhinishwaji ambapo hatua za uandaaji wa bajeti zimeainishwa, Miongozo ya uandaaji wa Bajeti ya Serikali, Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Bajeti za Taasisi za Serikali, Makadilio na Makisio ya Bajeti ya Serikali, nyaraka zinazopaswa kuwasilishwa Bungeni kuhusiana na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha husika, Mamlaka ya

Waziri wa Fedha kuwasilisha Bungeni ili Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa kila mwaka wa Fedha, Mamlaka ya Rais kuidhinisha Matumizi ya Serikali kabla yakuanza kutumika kwa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa kila mwaka wa Fedha, kipindi cha matumizi ya fedha za bajeti zilizoidhinishwa na Bunge na Rais kwa mwaka wa fedha, uwasilishwaji wa mambo muhimu ya sera za kibajeti na mapato ya Serikali, Mamlaka ya Bunge ya kuidhinisha Sheria ya Matumizi ya Serikali pamoja na Sheria ya Fedha kwa kila mwaka wa Fedha, Mamlaka ya Bunge kusitisha kibali cha matumizi kwa ajili ya fungu la Serikali, ukiukaji wa Serikali wa malengo ya kibajeti wakati wa dharura, kuweka utaratibu wa vyanzo na matumizi Mfuko wa Dharura, Mamlaka ya Waziri wa Fedha kusimamia Mfuko wa Dharura, taarifa za matumizi ya Mfuko wa Dharura, Mapato yatokanayo na Mfuko wa Dharura, Uhamishaji wa Fedha zilizotengwa katika Bajeti ya Serikali, Mapato ya Ziada na Mawasilisho ya Nyongeza ya Bajeti.

Sehemu ya Tano inabainisha masuala ya, utekelezaji, ufuatiliaji, tathimini na utoaji taarifa za bajeti ikiwemo Mamlaka ya kufanya matumizi, Idhini ya kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu, utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, Kibali cha matumizi kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, dhana ya Miadi, Miadi ya kifedha ya miaka mingi, mfumo wa udhibiti wa Miadi, mikataba ya Miradi ya Maendeleo, taarifa ndani ya mwaka wa fedha, taarifa za utekelezaji wa bajeti za robo mwaka na taarifa ya mwaka.

Sehemu ya Sita inahusu usimamizi wa mapato ambapo inabainisha misingi ya usimamizi wa mapato kwa ujumla na wajibu wa kukusanya na kusimamizi wa mapato.

Sehemu ya Saba inaweka utaratibu wa kusimamia fedha za bajeti kwa vyombo vya umma ikiwemo Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali zilizopo Nje ya Mfumo wa bajeti.

Sehemu ya Nane inahusu masuala ya kiujumla ikiwemo Mamlaka ya Waziri wa Fedha kuandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria ya bajeti, Mamlaka ya Bunge kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa za kibajeti Bungeni, uwajibishaji wa Mamlaka iliyoshindwa kutekeleza matakwa ya Sheria, hatua za urekebishaji dhidi ya Serikali na taasisi za umma, kinga kwa maafisa wa umma na masharti ya mpito.

Dar es Salaam,
27 Oktoba, 2014

**SAADA M. SALUM**
*Waziri wa Fedha*